# MINITI ZA KIKAO CHA WAKABIDHI 1 APRILI 2023

**Waliohudhulia**
Ingo Koll (Kipala) - Mwenyekiti
Anuary Rajabu - Katibu
Riccardo Riccioni
Antoni Mtavangu (Jadnapac)
Hussein Mmbaga
Justine Msechu
Clement Makangabila ( Czeus25 Masele)
Idd Ninga
Frank Kisamo

**Ajenda 1: Kufungua kikao**
Mwendeshaji wa kikao ndugu Ingo Koll, alifungua kikao na kutoa nafasi ya kujipendekeza kwa makatibu wa kikao, ambapo Anuary Rajabu na Ingo Koll wajitolea kuwa makatibu wa kikao, kwa ajili ya kurekodi miniti za kikao chenyewe.

**Ajenda 2: Kuangalia miniti za kikao kilichotangulia**
Miniti za kikao cha 04.Februari 2023 zilikubaliwa. Hapa wakabidhi walijadiliana na kukubaliana kuwa miniti za kikao chochote cha wakabidhi ziwekwe hadharani kwenye ukurasa wa jumuiya kwenye Wikipedia ya Kiswahili.

**Ajenda 3: Kupeana taarifa kuhusu kazi tuliyofanya, na yale ambayo tumeona**
Hapa kila mtu alipata nafasi ya kuelezea kuhusu kile kilichojadiliwa na kukubaliana kufanyia kazi katika kikao kilichopita.

Mtumiaji Riccardo; alisema kuwa yeye alijitahidi kukemea suala la Money akaunti, alitia nguvu kubwa katika hilo, ijapokuwa alikua na mujukumu mengi, lakini alijitahidi kila alipopata nafasi.

Mtumiaji Anuary Rajabu; alieleza kuwa alitia nguvu zaidi katika kukaribisha wageni, kwa kushirikiana na watumiaji wengine, kuhakikisha kuwa watumiaji wote waliojiandikisha kwenye Wikipedia ya Kiswahili wanapata salamu ya mwaliko, na mpaka sasa asilimia kubwa ya wote wamepata, pia alitia nguvu pia kwenye suala la kuboresha makala mbovu.

Mtumiaji Kipala; alisema kuwa alifika Arusha na kukutana na baadhi ya Wanawikipedia hapo, kama vile Idd ninga, Anuary Rajabu, Justine Msechu, Hussein m mmbaga na wengine, na kuweza kuelekezana mambo kadha wa kadha kama vile jinsi ya kutengeneza template, vigezo na kadhalika. Pia alitoa taarifa kwa Dumisani Ndubane wa Wikimedia Foundation aliyewahi kuuliza kuhusu kundi la University Students Wikimedia jinsi ilivyojadiliwa katika miniti za Februari. Aliona pia majaribio mbalimbali kuunda makala kuhusu watu wanaokosa umaarufu. Alifuta makala hizo na kuzuia waandishi kwa kuwakaribisha walete malalamiko wakiona si sawa lakini hakuna hata mmoja aliyepinga. Inaonekana ni ama mtu mmoja anayetumia akaunti tofauti au kampuni fulani ianyojaribu kuingiza watu kwenye wikipedia wakijaribu kuanza swwiki. Dalili yake ni makala yenye vyanzo finyu na hakuna makala kuhusu mhusika katika wikipedia nyingine kama enwiki..

Mtumiaji Idd ninga; alifanya doria na utafiti mfupi wa makala zilizo na tafsiri ya kompyuta, na kubaini zaidi ya makala 500, bado hukuna juhudi zozote ama mikakati ya namna gani ya kuzipunguza na kuziboresha makala hizo, Aidha Idd ninga alipendekeza kuwepo kwa mgawanyo wa makala hizo kwa wakabidhi kwa ajili ya maboresho. Idd aliombwa kuleta pendekezo jinsi ya kugawa makala hizo.

Pia watumiaji Czeus25 Masele (Clement),Hussein m mbagaa, Frank Kisamo walieleza kuwa walitia nguvu kubwa katika suala la ukaribisho wa wageni na kaboresha makala mbovu.

- 

**Ajenda 4: Mpango wa mwaka**
Hapa Antoni alitaja mada anazopenda kupeleka kwa Wikimedia Foundation kwa ajili ya kupata fedha za kuendesha editathons na mikutano (tazama mada alizotaja chini kwenye Nyongeza 1).
Riccardo alitoa tahadhari kuhusu mada ya gender studies akiona makala za Kiingereza hazifai kutafsiriwa moja kwa moja maana utamaduni wa Marekani ambako zinatungwa mara nyingi ni tofauti sana na mazingira ya Afrika ya Mashariki ambako wasomaji wetu wengi wanaishi.

Ingo (Kipala) aliona mada zote zilizoorodheshwa ni nzuri sana lakini aliona haiwezekani kushughulika zaidi ya mada 3 au 4 kwa mwaka mmoja hata tukijitahidi. Maana utekelezaji wa orodha hiyo ingehitaji semina na editathons lakini hatuna wahariri wa kutosha wenye uzoefu. Baada ya maarifa mabaya ya mwaka jana tulikubaliana utaratibu kuwa editathon ya wageni haiwezi kupeleka makala zake moja kwa moja kwenye nafasi ya makala bali kwenye nafasi ya watumiaji tu. Baadaye zinahitaji kuangaliwa. Alitaja muundo anayoona yeye inaweza kusaidia kukuza swwiki ukikazia zaidi kujenga maudhui yanayotafutwa na wasomaji wetu. (tazama Nyongeza 2).

**Ajenda 5: Mengineyo**
***Mapendekezo***
Uchaguzi mpya wa wakabidhi ( Riccardo alipendekeza )
Suala hili lilikubaliwa na wakabidhi wote, kuwepo kwa uchaguzi mwezi huu Aprili 2023, kuziba nafasi ya wakadhi ambao wamejitoa kwenye ukabidhi. Kipala alisema ataandaa utaratibu mzima wa uchaguzi kwa kutangaza kwa watumiaji waliojiandikisha wote.
Pamoja na uchaguzi tupige pia kura kuhusu utaratibu wa kuchaguliwa: “**mgombea wa ukabidhi apate zaidi ya nusu ya kura zote zinazopigwa wakati wa uchaguzi.”**
**Ajenda 6: Kufunga kikao**
Mwisho mwenyekiti alifunga kikao na kutoa shukrani kwa wahudhuriaji wote.

Anuary Rajabu   Ingo Koll

Waandishi

**<u>Nyongeza 1: Mada zilizoandaliwa na Antoni / kwa ajili ya mpango wa mwaka</u>**
(Namba za Antoni zilikuwa tofauti)
1 Education  - Wiktionary kukuza  editathons kuhusu education
2 Wiki for university -  kuingiza wanavyuo
3 Gender inclusion
4 Art and feminism
5 Wiki for refugees
6 Teknolojia - wiki loves astronomy
7 Wiki loves stem makala kuhusu teknolojia

8 Wiki developers upande wa Tanzania - software development (infoboards templates)
9 GLAM maktaba na makumbusho
10 Kuongeza makala swwiki na enwiki
11 Kuongeza picha kwa makala zinahitaji picha
12 Picha za kata
13 Afya
14 Culture - sauti za busara , film festival, michezo
15 Community engagement - kuanzisha kundi upande wa zanzibar
16 Entertainment michezo wiki loves sport, wiki loves Music
17 Wiki for universities - upande wa tanzania na Kenya na SADCC
18 Sustainable development goals - mazingira, maji,
19 Inclusion ujumuishwaji , haki za kibinadamu,
20 Registration wa user group mbele ya serikali kwa kurahisisha miradi -
21 Regional collaboration - told cities project urithi wa nchi za kiafrika

**Nyongeza 2: Mada zilizotajwa na Ingo / kwa kazi ya mwaka**

Mkazo uwe kwenye mada zinazotafutwa na wasomaji wetu. Ni hasa zile zinazohusu Tanzania na Afrika, pamoja na mada za lugha ya Kiswahili na kuhusu afya

1. Kutafsiri makala kuhusu Tanzania na Afrika Mashariki zilizopo kwenye enwiki. Ziko nyingi, ni rahisi kuanza kwa kupitilia categories za enwiki
2. Makala za Afya zipo lakini zinahitaji masahihisho (ni matokeo ya mradi wa kimataifa)
3. Tuna pengo katika eneo la michezo, ila hatuna wataalamu katika eneo hili
4. Kukamilisha Wabunge wa Tanzania (hata kama ni watu wa kupita, ni mazoezi mazuri)
5. Picha za Kata za Tanzania (tukipata fedha kutoka WmF)
6. Kama serikali inaweka data za sensa hadharani: kata na wilaya za Tanzania (kazi kubwa sana)